*Kiob cha Lugha*
*Juzuu 1, Na. 2 (1995)*

# DHANA ZA UMAPOKEO NA USASA KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI

S.M. Sanka

## 1.0 Utangulizi

Mgogoro wa ushairi wa Kiswahili uliojitokeza mwanzoni mwa miaka ya 1970 umewagawa washairi wa Kiswahili katika makundi makuu mawili. Makundi hayo ni ya washairi wanamapokeo na wanausasa. Washairi wa kundi la wanamapokeo ni wale wanaozingatia ulinganifu wa vina na mizani katika ushairi wa Kiswahili. Washairi wa kundi la wanausasa, kwa upande mwingine, ni wale wasiozingatia ulinganifu wa vina na mizani (Senkoro,1988:3). Kutokana na mgawanyiko huo tunapata makundi mawili ya mashairi. Makundi hayo ni ya mashairi ya mapokeo na mashairi ya kisasa. Makala hii inakusudia kujadili utata unaotokana na dhana hizo za *umapokeo* na *usasa* zilizotumika kuyaainisha mashairi ya Kiswahili katika makundi hayo. Kwanza, tutajadili kwa ufupi dhana za *umapokeo* na *usasa* katika fasihi za Ulaya na Marekani kwa ufupi. Pili, tutajadili dhana hizo kama zilivyotumika katika kuainisha ushairi wa Kiswahili. Tatu, tutajadili utata unaotokana na dhana za *umapokeo* na *usasa* katika ushairi wa Kiswahili. Hatimaye tutatoa majumlisho yatokanayo na mjadala huo.

## 2.0 Dhana za Umapokeo na Usasa Katika Fasihi

*Umapokeo* ni dhana inayoelezea utaratibu na misingi ya kisanaa iliyozoeleka na kuchukuliwa kama kanuni au sheria na wasanii wa sanaa inayohusika. Kanuni hizo hutumika kama kipimo cha kupimia ubora wa sanaa hiyo. Msanii yeyote anayetaka kusana kazi yake hulazimika kuzingatia kanuni hizo. Kwa hivyo kazi yake lazima ifanane na za wasanii maarufu waliotangulia. Hivi ni kusema kwamba msanii huyo anapokea kunga za sanaa kutoka kwa waliomtangulia. Kutokana na hali hiyo wasanii wanaofuata utaratibu huo wa kimapokeo huitwa *wanamapokeo.*

Katika fasihi, umapokeo ulijidhihirisha zaidi katika ushairi. Ushairi ndiyo sanaa ya fasihi iliyo kongwe zaidi.Ulinganifu wa vina na mizani ulichukuliwa kama sifa za shairi bora. Aidha washairi walielekezwa maudhui ya mashairi yao. Mathalani Plato (Smiths and Parks, 1951) alisisitiza kuwa washairi lazima watunge mashairi yanayotukuza Miungu na kusimulia sifa za watu mashuhuri. Anasema:

> ...We must remain firm in our conviction that hymns to the Gods and praises of famous men are the only poetry which ought to be admitted into our state (Smith & Parks, Eds. 1951:22)

Tafsiri:

> *Lazima tushikilie msimamo wetu kwamba mashairi ya kutukuza Miungu na sifa za watu mashuhuri ndiyo mashairi pekee yanayopaswa kuruhusiwa katika dola yetu* (Tafsiri ni ya mwandishi)

Hivyo tunaweza kusema kwamba mashairi ya mapokeo ni yale yanayofuata kanuni mahususi za fani na maudhui. Kanuni hizo ni pamoja na urari wa mistari vina na mizani. Aidha ushairi wa kimapokeo unaonekana kufungamanishwa na imani za kidini kama inavyoonekana katika dondoo hiyo hapo juu.

Usasa (modernism), kwa upande mwingine, ni dhana inayotumika kubainisha mabadiliko katika sanaa ambayo yanakiuka kanuni za kimapokeo. Kamusi ya istilahi za kifasihi ya Abrams (*A Glossary of Literary Terms*:1981:109) inaelezea usasa kama istilahi inayotumika kubainisha maudhui, maumbo, na mitindo mipya katika fasihi na sanaa kuanzia baada ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia, yaani mwaka 1914. Ufafanuzi kama huu pia unatolewa katika Kamusi ya Istilahi za Kifasihi ya Beckson na Ganz (1989:164-165). Kamusi hiyo inaendelea kufafanua kuwa usasa unajibainisha kwa kutupilia mbali mitindo na mbinu za kifasihi za kipindi kilichotangulia na kupinga kwake maadili ya kijamii na kiuchumi ya kibwanyenye. Kadhalika, *The Cambridge Paperback Encyclopedia* (1995:570) inauelezea usasa kama mbinu za majaribio katika fani mbalimbali za sanaa katika kipindi cha mwanzo cha Karne ya 20. *Encyclopedia* hiyo inaongezea kwamba majaribio hayo yalichochewa na kanuni za kimapokeo za kisanaa zilizokuwepo na mashaka juu ya nafasi na mustakabali wa binadamu katika ulimwengu.

Fafanuzi zote zilizotolewa hapo juu zinaonesha kwamba *usasa* ulijitokeza mwanzoni mwa karne ya 20; unakiuka mitindo na mbinu za kisanaa zilizokuwepo; na maudhui yake yanapinga mfumo wa kijamii na kiuchumi uliokuwepo.

## 3.0 Umapokeo na Usasa Katika Ushairi wa Kiswahili

Mashairi ya Kiswahili yamegawanyika katika makundi makuu mawili kama tulivyodokeza katika utangulizi. Makundi hayo ni ya mashairi ya mapokeo na mashairi ya kisasa. Mashairi ya mapokeo ni yale ambayo yanazingatia kanuni za urari wa vina na mizani. Mashairi ya Kisasa, kwa upande mwingine, ni yale yasiyofuata kanuni hizo za urari wa vina na mizani. Kutokana na fafanuzi hizi inaonekana kuwa urari wa vina na mizani ndiyo kigezo pekee kinachoyagawa mashairi ya Kiswahili katika makundi haya mawili.

Inawezekana kuwa uainishaji huu unatokana na mgogoro wa ushairi uliochochewa na sababu za kinadharia kuhusu maana ya jumla ya shairi na maana ya shairi la Kiswahili (Senkoro, 1988:3). Kutokana na jinsi wanafasihi wanavyoelewa maana ya shairi na maana ya shairi la Kiswahili yamepatikana makundi mawili. Kundi moja ni lile linaloona shairi la Kiswahili kama aina ya sanaa inayotumia lugha ambapo kuna mlingano wa vina, mistari, na mizani. Utungo wowote ambao haufuati kanuni hizi tulizotaja hapo juu siyo ushairi wa Kiswahili kufuatana na mtazamo wa kundi hili. Mashairi yanayofuata kaida za urari wa vina na mizani huitwa mashairi ya mapokeo. Mashairi haya yanaitwa mashairi ya mapokeo kwa sababu kanuni za utunzi wake zimeainishwa rasmi na huwa zinatakiwa kufuatwa na mtu anayetaka kutunga shairi la Kiswahili. Kwa mfano, Kaluta Amri Abeid (1954) aliandika kitabu kinachohusu sheria za kutunga mashairi. Sheria hizi ni lazima zifuatwe na kila anayetaka kutunga shairi la Kiswahili. Mambo makuu ya msingi katika sheria hii ni ulinganifu wa vina na mizani. Mambo haya yanasisitizwa vile vile na malenga maarufu wa Kiswahili kama vile Shihabdin Chiraghdin (1971), Saadan Kandoro (1978),Jumanne Mayoka (1984), Ibrahim Noor Shariff (1988), na wengineo. Shihabdin Chiraghdin (1971: 12-14) akisisitiza sifa za shairi la Kiswahili anasema:

> Ili shairi liwe shairi, lisiwe mvurugano wa maneno tu ambao wakerezakereza katika masikizi na kueleza moyo, lazima liwe na ulinganifu wa mizani, vina na lugha iliyo tukufu yenye kuvuta masikizi na fikira kama ambavyo sumaku huvuta chuma. . . . tungo zisizofuata ulinganifu wa vina na mizani zikikubaliwa kuwa ni mashairi basi ushairi wa Kiswahili utakuwa umeanguka kitakotako.

Mkabala huu wa Chiraghdin unamaanisha kuwa ulinganifu wa vina na mizani ni jambo la lazima katika ushairi wa Kiswahili. Shairi la Kiswahii haliwi shairi mpaka liwe na ulinganifu wa vina

na mizani. Na anashawishi kuwa tungo zisizo na ulinganifu wa vina na mizani zisikubaliwe kuwa mashairi vinginevyo ushairi wa Kiswahili utaanguka kitakotako. Mkabala huu unaungwa mkono na Jumanne Mayoka (1984: x) ambapo katika utangulizi wa kitabu chake, *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*, anasema:

> Kufuatana na mtazamo huu, usanaa wa shairi la Kiswahili uko katika ulinganifu wa vina na mizani pekee. Kutokana na sababu hiyo malenga hawa wamethubutu kudai kuwa vina na mizani ni uti wa mgongo wa mashairi ya Kiswahili (Mayoka, 1984: 5-6).

Mayoka (1984: 21) anadai kwamba vina ni utamaduni wa Kiswahili na Wabantu wengine pia. Kwa hiyo muundo wa mashairi wenye ulinganifu wa vina na mizani ambao ameutumia kwenye diwani yake ni wa asili ya Kibantu. Anatoa hoja hiyo ili kulipa nguvu dai lake kwamba washairi wanaotunga tungo zisizo na ulinganifu wa vina na mizani wameathiriwa na tungo za kigeni, yaani Kiingereza. Dai hili ni vigumu kukubalika. Ingawa ni kweli kwamba kulikuwa na ulingano wa vina na mizani kwa kiwango fulani katika ushairi wa Kibantu (Gibbe, 1981), muundo huo haukuwa sheria. Aidha muundo wa ulinganifu wa vina na mizani siyo mahususi kwa ushairi wa Kiswahili na wa Kibantu pekee. Fasihi za jamii mbalimbali ulimwenguni zilikuwa na miundo kama hiyo. Ulinganifu wa vina na mizani ulisisitizwa pia katika jamii za Kigiriki za kale (Smiths & Parks, Eds. 1951). Kwa hiyo ni vigumu kuutambulisha ushairi wa Kiswahili kwa kigezo cha ulinganifu wa vina na mizani pekee.

Kundi lingine ni lile linaloitwa la wanausasa. Kundi hilo linajumuisha washairi ambao wanatunga mashairi yasiyofuata kanuni za urari wa vina na mizani. Watetezi wa kundi hili ni pamoja na Mulokozi na Kahigi (1973, 1979), Kezilahabi (1974) na Senkoro (1988). Washairi hawa wanaamini kuwa vina na mizani siyo *uti* wa mashairi ya Kiswahili. Mathalani, Mulokozi na Kahigi (1979: 9-10) na Senkoro (1988: 10-11) wanasema kwamba ushairi wa Kiswahili haubainishwi kwa urari wa vina na mizani. Wanasema hivyo kwa sababu vina na mizani si sifa pekee za ushairi wa Kiswahili. Mulokozi na Kahigi (1979:25) wanafafanua ushairi kama:

> Sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu wa maneno fasaha na yenye muwala, kwa lugha ya mkato, picha au sitiari au ishara, katika usemi, maandishi, au mahadhi ya wimbo, ili kueleza wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisi fulani, kuhusu maisha na mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo.

Maana hii ya ushairi iliyotolewa hapo juu inajumuisha mashairi yanayofuata ulinganifu wa vina na mizani na yale yasiyofuata ulinganifu huo pia. Hapa urari wa vina na mizani hauchukuliwi kama kitambulisho pekee cha ushairi na mashairi ya Kiswahili. Pamoja na hivyo wanazuoni hawa nao wametumia urari wa vina na mizani kuwa mstari unaotenganisha mashairi ya *mapokeo* na mashairi ya *kisasa*. Watetezi wa kundi la wanausasa, pamoja na kwamba hawapingi ushairi wa kimapokeo kuwa ni ushairi wa Kiswahili, wanatambulisha mashairi yao kuwa ni ya kisasa kwa vile tu hayazingatii kanuni za ulinganifu wa vina na mizani. Aidha mjadala uliokuwepo baina ya makundi haya ulikuwa umeegemea zaidi kwenye suala la ulinganifu wa vina na mizani na kuacha vipengele vingine vya msingi katika ushairi. Hali hii inasababisha utata mkubwa katika dhana za *umapokeo* na *usasa* zilizotumika katika uainishaji huu kama tutakavyoona hapo chini.

## 4.0 Utata Utokanao na Dhana za *Umapokeo* na *Usasa*

Dhana hizi mbili, *umapokeo* na *usasa*, zinaleta maswali mengi kwa yeyote anayedadisi kunga za ushairi na mashairi ya Kiswahili. *Umapokeo* na *usasa* uko katika nini hasa.Tunaweza kujiuliza kuwa mapokeo tunayozungumzia ni kuanzia lini? Ni aina ipi ya ushairi ulio mkongwe zaidi?

Ushairi unaofuata kanuni za urari wa vina na mizani au ule usiofuata kanuni hizo? Ukongwe wa aina ya ushairi pekee unatosha kuyaweka mashairi ya Kiswahili katika makundi haya?

Inaonekana dhahiri kuwa kigezo cha urari wa vina na mizani hakitoshelezi kubainisha mashairi kuwa ya mapokeo. Tunasema hivyo kwa sababu kuna baadhi ya mashairi ambayo muktadha wake wa kihistoria ni wa kipindi kilichopo lakini yanazingatia kanuni za ulinganifu wa vina na mizani. Mathalani, baadhi ya mashairi ya Said Ahmed Mohamed (1980) katika diwani yake ya *'Sikate Tamaa* yanazungumzia mambo yanayohusu jamii yetu katika kipindi hiki cha historia lakini yanazingatia kanuni za urari wa vina na mizani. Kwa mfano mashairi kama vile; *Watoto wa Afrika (uk.2), Nawaita Washairi (uk.3), Nyoosha Mkono (uk.16), na Naandika!* ( uk.17). Mashairi haya yanazingatia ulinganifu wa vina na mizani, lakini yanazungumzia mambo ya zama hizi. Abdilatif Abdalla (1980: ix) anabainisha muktadha wa kihistoria wa mashairi hayo ambayo yanahusu matukio ya baada ya uhuru katika dondoo lifuatalo hapa chini:

> . . . mtunzi wetu huyu amejasiri; na nimelitumia neno 'amejasiri' kwa makusudi kwa sababu tangu hizi nchi zetu zipate uhuru, yajapo mambo yahusianayo na siasa, Fasihi ya Kiswahili imekuwa ikizungumzia na kujishughulisha zaidi na uchambuzi wa yaliyokuwa yakitendwa na wakoloni walipokuwa wametutawala na imekuwa ikiyafumbia macho yale maovu na makosa tuyatendayo sisi wenyewe .

Dondoo hilo hapo juu linaonesha kuwa mashairi hayo ya Said Ahmed Mohamed yanazungumzia mambo ya kipindi cha kihistoria kilichopo. Yaani kipindi cha baada ya uhuru. Tunaweza kushawishika kuyaweka mashairi hayo katika kundi la mashairi ya kisasa, lakini haiwezekani kwa vile yanazingatia kanuni za kimapokeo za ulinganifu wa vina na mizani. Kwa hali hiyo tutakuwa hatujafanikiwa kutofautisha mashairi ya mapokeo na ya kisasa. Kwa hivyo ni dhahiri kuwa ulinganifu wa vina na mizani hautoshelezi kuyaainisha mashairi ya Kiswahili katika makundi ya mashairi ya mapokeo na mashairi ya kisasa.

Utata mwingine kuhusu dhana za *umapokeo* na *usasa* unahusiana na suala la wakati. Hapa tunajiuliza kuwa *mapokeo* ya kanuni za mashairi ya Kiswahili za urari wa vina na mizani yalianza lini? Ibrahim Noor Shariff (1988: 189) anadai kuwa kanuni za kimapokeo za ulinganifu wa vina na mizani zilianzia kwa Fumo Liyongo wa Baury kabla ya karne ya kumi na nne. Akitetea hoja hiyo, Shariff anasema:

> Tuna ushahidi wa kutosha wenye kutuonesha mtungaji wa awali wa Kiswahili ambaye tungo zake tunazo ni Fumo Liyongo wa Baury, ambaye kwa ushahidi tulionao inaonesha kuwa aliishi kitambo kabla ya karne ya kumi na nne. Pili, hakuna ushahidi wowote wa tungo za "Kibantu" za zamani kushinda za Fumo Liyongo. . . . Fumo Liyongo na watungaji wazito wa Kiswahili walioishi baadaye hawakutunga bila ya vina na wengi hawakutunga bila ya vina na mizani.

Dai kwamba ushairi wa Kiswahili unaozingatia kanuni za ulinganifu wa vina na mizani ulianzia kwa Fumo Liyongo kabla ya karne ya kumi na nne linatupa mashaka. Kwanza, utafiti wa Mulokozi na Sengo (1995: 29) umebainisha kuwa tarehe ya mashairi ya Fumo Liyongo inatatanisha. Wakati ambapo watu waliohojiwa wanasema kuwa Fumo Liyongo aliishi kabla ya karne ya kumi na tatu, shairi lake la kale zaidi lililopo ni la mwanzoni mwa karne ya kumi na sita (1517 A.D.) ambalo linaitwa "Swifa ya Mwana Manga" au "Kumsifu Yanga". Pili, kutegemea ushahidi wa mashairi andishi kuamua tarehe ya ushairi wa Kiswahili na chimbuko la kanuni zake za sanaa kunaweza kupotosha ukweli. Siyo sahihi kuamua kwamba maadamu hakuna

ushahidi wa mashairi yaliyoandikwa kabla ya Fumo Liyongo basi ushairi haukuwepo kabla ya hapo. Haiyumkiniki kama ni kweli kwamba hakuna mtu yeyote aliyetunga mashairi kabla ya Fumo Liyongo. Bila shaka Waswahili walikuwa na fasihi yao kabla ya kuingia kwa fani ya uandishi. Na kwa kawaida fasihi simulizi ni mali ya jamii ambayo haihusishwi na mtunzi binafsi. Kwa hali hiyo inawezekana kuwepo kwa watunzi wengine wa mashairi katika jamii ya Waswahili kabla ya Fumo Liyongo. Hivyo siyo sahihi kudai kuwa Fumo Liyongo ndiye mtungaji wa awali wa mashairi ya Kiswahili.

Kutokana na dai la Shariff, inawezekana mapokeo yanaanzia kwa Fumo Liyongo, na hasa pale fani ya uandishi ilipoanza kutumika katika kutunga mashairi ya Kiswahili. Lakini wanamapokeo wanatukanganya hapa. Mayoka (1984: x) anadai kuwa ushairi wa mapokeo ni wa *asili ya Kibantu.* Lakini fani ya uandishi ni ngeni kwa Wabantu. Kwa hiyo ushairi wa Kiswahili, ambayo ni lugha ya Kibantu, ulikuwepo kabla ya kuingia kwa fani ya uandishi. Aidha hakuna uthibitisho kuwa mashairi ya asili ya Kibantu yalikuwa yanasisitiza kanuni za urari wa vina na mizani. Kwa mfano, Mulokozi na Kahigi (1979:10-12) na Balisidya (1987:15) wanaeleza kuwa Waswahili wana mashairi yasiyozingatia ulinganifu wa vina na mizani ingawa mitindo na miundo hiyo ilikuwepo na kupendwa na watu. Mulokozi na Kahigi (1979:12) wanathibitisha hoja yao kwa mfano ufuatao:

> Silie mama silie
> Ukalia waniliza
> Wanikumbusha makiwa
> Makiwa ya baba na mama
> Baba na mama watende
> Wanioza dume kongwe
> Halisafiri halendi
> Kazi kumeza matonge.

Shairi hili la fasihi simulizi lina mlingano wa vina kwa kiasi fulani. Lakini hakuna ulinganifu wa mizani unaoshabihiana na ule upatikanao katika mashairi ya mapokeo. Mashairi mengi ya fasihi simulizi yana miundo kama hiyo (Gibbe, 1981). Kwa hiyo ni dhahiri kabisa kwamba ulinganifu wa vina na mizani haukuwa sheria katika ushairi wa Kiswahili.

Inaonekana kuwa ushairi usiozingatia kanuni za ulinganifu wa vina na mizani uko karibu zaidi na ushairi wa fasihi simulizi. Kama hivyo ndivyo ilivyo, ushairi huo una ukongwe zaidi kuliko ushairi wa mapokeo. Ikiwa mashairi yanayokiuka kanuni za urari wa vina na mizani ni makongwe zaidi kuliko mashairi ya mapokeo ambayo yanafuata kanuni hizo, ni kwa vipi yanaitwa ya kisasa?

Mulokozi na Kahigi (1979: 3) wanakiri ukongwe wa *mashairi ya kisasa*. Kwa maneno yao wenyewe wanasema:

> . . . si miundo yote ya sanaa inayopendekezwa kutumika sasa ni mipya; baadhi ni ya kale iliyokuwa imesahauliwa na ambayo sasa inafufuliwa kwa sababu inaweza kubeba maudhui ya leo. Baadhi ni miundo ya kawaida ya kifasihi simulizi ambayo inaingizwa katika fasihi andishi ya Kiswahili.

Kufuatana na kauli hiyo hapo juu, tunaweza kusema kwamba usasa wa mashairi yasiyofuata kanuni za ulinganifu wa vina na mizani unahusishwa na tarehe ya kuingizwa kwake katika fasihi andishi. Mashairi ya aina hii yalichapishwa siku za baadaye tofauti na mashairi ya kimapokeo ambayo yalianza kuchapishwa zamani. Kumbukumbu zinaonesha kuwa mashairi yasiyofuata

kanuni za urari wa vina na mizani yalianza kuchapishwa baadaye kuliko mashairi ya mapokeo. Mengi ya mashairi hayo yalianza kuchapishwa kwenye miaka ya 1970. Mathalani, diwani ya Mulokozi na Kahigi iitwayo *Mashairi ya Kisasa* ilitoka mwaka 1973. Diwani ya Kezilahabi, *Kichomi*, ilitoka mwaka 1973. Kuchelewa kuingia katika maandishi kwa mashairi ya aina hii hakutoshi kuyafanya mashairi hayo kuitwa ya kisasa. Hii ni kwa sababu mashairi yasiyofuata kanuni za urari wa vina na mizani yalikuwepo kabla ya kuingia kwa taaluma ya uandishi katika Afrika ya Mashariki. Washairi wa kundi la wanausasa hawakubuni sanaa mpya ambayo haijawahi kuwepo katika historia ya ushairi wa Kiswahili. Kitu walichofanya ni kurejesha aina ya sanaa ambayo ilibaguliwa katika uandishi na kufanya iandikwe. Hali hii haifanyi sanaa hii kuwa ya kisasa.

Inavyoonekana usasa wa mashairi ya kisasa uko katika uhuru wa mshairi kutumia aina ya mitindo na miundo ya kisanaa anayopendezwa nayo. Tunasema hivyo kwa sababu watetezi wa usasa hawaukani muundo wa vina na mizani katika ushairi wa Kiswahili. Wanachopinga ni kuufanya muundo huo kuwa sheria inayopasa kufuatwa na kila msanii kama wanavyotaka wanamapokeo. Mulokozi na Kahigi (1979: 10-11) wanauweka wazi msimamo huo kwa kusema:

> Msimamo wetu ni kwamba hakuna muundo au miundo maalum ambayo lazima ivaliwe na kila shairi, au sheria maalum zisizotanguka ambazo lazima zikaririwe na kila mshairi kama "sala ya bwana".

Kutokana na hali hiyo ni wazi kwamba kigezo cha ulinganifu wa vina na mizani hakitoshelezi kupambanua mashairi ya mapokeo na ya kisasa. Kwa hiyo tunapotaka kuainisha mashairi ya Kiswahili kuna haja ya kutazama vigezo vingine zaidi ya ulinganifu wa vina na mizani.

## 5.0 Hitimisho

Katika makala hii tumeona mambo yafuatayo: kwanza, urari wa vina na mizani pekee hautoshi kuugawa ushairi wa Kiswahili katika makundi ya ushairi wa mapokeo na wa kisasa. Hii ni kwa sababu kuna mashairi yanayozingatia kanuni za ulinganifu wa vina na mizani yanayozungumzia mambo yanayohusu kipindi cha sasa cha kihistoria.

Pili, kuchelewa kuingia katika fasihi andishi kwa mashairi yasiyofuata kanuni za urari wa vina na mizani hakutoshi kuyafanya mashairi hayo kuwa ya kisasa. Tunasema hivi kwa sababu kuna ushahidi wa kutosha kuwa mashairi yasiyofuata urari wa vina na mizani yalikuwepo kabla ya kuingia kwa maandishi katika jamii za Kiswahili.

Tatu, tumeona kuwa mashairi ya kisasa ni yale yanayozingatia uhuru wa mshairi katika kutunga mashairi yake. Washairi wanaofuata mkabala huu wa mawazo wanaweza kuitwa wanausasa katika msingi huo.

Hivyo, tunaweza kusema kwamba mashairi ya Kiswahili yanapaswa kuainishwa kwa vigezo vinavyozingatia sifa za jumla za mashairi kama zilivyoainishwa na Mulokozi na Kahigi (1979) na Said Ahmed Mohamed (1990). Pamoja na kuzingatia sifa hizo pia kuna haja ya kuzingatia kipindi cha kihistoria ambacho mkabala wa kifasihi unaotetea uhuru wa mshairi kuteua fani anayoitaka uliibuka. Kwa kuwa mkabala huo unaotetea mashairi yasiyofuata kanuni za urari wa vina na mizani ulianza kujitokeza mwanzoni mwa miaka ya 1970, tunaweza kusema kuwa usasa unaanzia wakati huo.

## Marejeo


Abdalla, A. ( Mhr.), "Utangulizi" katika *'Sikate Tamaa* (Tungo za Said Ahmed Mohamed.) . Longman Kenya, Nairobi. 1980

Abeid, K.A., *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*, East Africa Literature Bureau, Dar es Salaam. 1954

Abrams, M. H. , *A Glossary of Literary Terms* (Toleo la 4.): Holt, Rinehart and Winston, New York. 1981

Balisidya, N. M. , " Adopted or Adapted? Neo Swahili Oral Literature in Tanzania. *Kiswahili:* Vol. 54/1&2 , University of Dar es Salaam, Dar es Salaam. 1987

Beckson, K.and A. Ganz, *Literary Terms: A Dictionary* (Toleo la 3), The Noonday Press. New York, 1989

Chiraghdin, S. na Wenzake, "Tarehe ya Ushairi wa Kiswahili" *Mulika* Na. 7, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 1975.

Chiraghdin, S "Utangulizi" katika Nasir, A., *Malenga wa Mvita*, O.U.P. Nairobi. 1971.

Crystal, D. (Ed.), *The Cambridge Paperback Encyclopedia* Cambridge University Press, Cambridge. 1995.

Gibbe, A. G., Fasihi na Jamii: Baadhi ya Washairi wa Kiswahili; 1960-1977, *Kiswahili*, Vol. 48/1, 1978

-------------, "Vina Katika Ushairi wa Kiswahili", TUKI, Dar es Salaam, 1981.

Kahigi, K.K. "Ushairi: Mtazamo wa Kisayansi" *Kiswahili* Vol. 45/1. TUKI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam. 1976.

Kandoro, S.A. *Ushahidi wa Mashairi ya Kiswahili*, Longman Tanzania, Dar es Salaam. 1978.

Kezilahabi, E., *Kichomi*, Haineman, Nairobi. 1973.

Mayoka, J.M. *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*, T.P.H. Dar es Salaam. 1984

Mohamed, S. A. , *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi*. Evans Brothers (Kenya) Limited, 1990

Mulokozi, M.M., "Ushairi wa Kiswahili ni Nini? *Lugha Yetu*, Vol. 25 BAKITA, Dar es Salaam. 1975.

-----------------------, "Revolution and Reaction in Kiswahili Poetry" in *Kiswahili*, Journal of The I.K.R. Vol.45/2, University of Dar es Salaam. 1975.

______________ na K.K. Kahigi (1973). *Mashairi ya Kisasa*. T.P.H. Dar es Salaam.

-------------------------------------, *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam. 1979

Mulokozi, M. M. na T.S.Y Sengo, *History of Kiswahili Poetry (A.D. 1000 - 2000)*. I.K.R. University of Dar es Salaam. 1995

Topan, F. (1973), "Dibaji" katika E. Kezilahabi, *Kichomi*, Haineman. Nairobi.

Senkoro, F.E.M.K. (1980). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*, DUP, Dar es Salaam.

Smith, J. H. and E. W. Parks (Eds.), *The Great Critics: An Anthology of Literary Criticism*. W.W. Norton & Company Inc. New York, 1951.

Spears, M. K. , *Dionysius and The City: Modernism in 20th Century Poetry*. Oxford UniversityPress. 1970.